Vijana Wanaoishi Sehemu za Mashambani wanaweza kuwa Wajasiriamali wa kesho

Nteranya Sanginga ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki

Ibadan, Nigeria, Februari 9 2016 (IPS) – Ukuzaji wa ustawi kote barani Afrika ndio msingi wa uwezo wa ulimwengu kuafikia ahadi zake za kukomesha umaskini na njaa kufikia mwaka wa 2030.

Nteranya Sanginga, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (International Institute of Tropical Agriculture - IITA). Picha ni kwa hisani ya IITA

Idadi kubwa ya ongezeko la watu inachangia katika changamoto hii, na pia inatupaa mbinu ya kutumia kuangamiza umaskini na njaa.

Katika miongo mitatu iliyopita, idadi ya watu barani Afrika imeongezeka mara tatu. huku uibukaji wa miji umeongezeka kwa kasi mno, hali hii haijapunguza idadi ya watu wanaoishi katika sehemu za mashambani. Hili linadhihirika kutokana na namna uzalishaji katika kilimo umeongezeka kwa kasi zaidi kuliko kama ilivyo ukuaji wa kilimo duniani kote, lakini ukuaji huu sio wa haraka ili kuweza kutatua hali kinzani ya bara la Afrika. Bara lenye ardhi ya kulimwa ambayo haijatumika huku bara lenyewe likisalia kuwa bara linaloagiza chakula kutoka mataifa ya nje.

Huu ndio ukweli. Ukweli huu unarejelea kanuni fulani msingi: kwanza Afrika ina uwezo mkubwa, lakini maendeleo lazima yajumuishe sekta za maeneo ya mashambani na sekta za kilimo. Kulingana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa, wakulima wadogo wanachangia asilimia 80 ya chakula katika eneo la Afrika Kusini mwa Janga la Sahara. Na kwamba wakulima hawa wadogo ndio wajasiriamali muhimu ambao lazima wawezeshwe ili kuzalisha mapato, kazi na nafasi za ukuaji.

Mengi yanafanywa na serikali na mashirika ya kimataifa kuboresha usalama wa chakula, hii ni kupitia programu zinazolenga ulinzi wa jamii na programu zinaozlenga maendeleo katika sekta ya kilimo.

Kile ambacho sisi katika Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) tunafikiria ni muhimu ni kwamba watu wenyewe wanahitaji kuwezeshwa ili kuweza kutumikiza uwezo wao na uwezo wa bara lao.

Ingawa sera za umma na mikakati mikubwa ya sekta ya kibinafsi zina nafasi yake katika kutekeleza haya, uwezeshaji wa watu wa bara la Afrika ni muhimu.

Kimsingi, hili ni jambo la kawaida. Lakini jukumu letu kuu ni kuongoza ushirikiano wa utafiti katika kuibua suluhisho kwenye sekta ya kilimo, suluhisho za kushughulikia njaa na umaskini katika eneo hili, maono yetu yanayotokana na mawazo kwamba viunganishi vya baadhi ya mikakati mbalimbali inayoshughulikia ardhi havijaratibiwa ifaavyo, viunganishi hivi ni wajasiriamali.

Ukulima wa familia unaofanywa na familia ndio wenye wawekezaji wakubwa zaidi katika kilimo. Pia, shughuli za biashara kutoka mashinani ndizo njia kuu za kukuza utendakazi.

Hii ndiyo sababu Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) inaeneza Jukwaa lake la Ukuzaji katika Biashara (Business Incubation Platform), mfumo wenye uhusiano wa karibu na programu zetu za Vijana Wafanyabiashara-Kilimo (Youth Agripreneurs) na ambazo hulenga kuwezesha utoaji wa huduma muhimu na zenye thamani kwa

haraka. Mwelekeo wetu ni wa ushirikishi ambao unalenga kuboresha uzalishaji na kutoa fursa zenye manufaa kwa vijana, hasa vijana wanaoishi katika sehemu za mashambani.

Sio vijana wote wanaweza kuhamia mijini: na ikiwa vijana watafanya hivyo, maeneo ya mashambani yataumia kutokana na idadi kubwa ya wazee watakaosalia mashambani wakifanya kazi.

Ninasisitiza kwamba lengo hapa ni kuzalisha pesa na sio tu kuzitumia! Ninasisitiza hili ili niweze kufikisha ujumbe kwamba uendelevu wa kweli unahitaji mitandao faafu ambayo inaweza kuhakikisha mawazo yanayotokana na utafiti yanatimizwa na kuzalisha matunda.

Zingatia NoduMax, mmojawapo ya maendeleo katika Jukwaa letu la Ukuzaji katika Biashara (Business Incubation Platform). NoduMax ni dawa ya nafaka ya soya ambayo huwezesha upatikanaji zaidi wa naitrojeni hewani – hali ambayo hatimaye huboresha uzalishaji wa udongo – na hivyo basi kuongeza mazao hadi kilogramu 450 zaidi ya soya kutoka kila hektari. NoduMax, ni rahisi kutumia na inapatikana kwa bei nafuu.

Teknolojia hii ilitayarishwa na Jukwaa letu la Ukuzaji katika Biashara mjini Ibadan. Sasa wakati umefika wa kuitengeneza NoduMax kwa idadi kubwa na kuiuza duniani kote. Hizi zote ni mbinu za uendelevu za kukuza uzalishaji wa kilimo na kuimarisha usalama zaidi wa chakula, na manufaa yake ni kwamba huhitaji kulima zaidi au kumiliki ardhi mpya.

Pia tunaandaa aina mbalimbali za Aflasafe ili kukumbana na aflatoksini ambazo zimekuwa janga kubwa kwa vyakula vinavyoliwa zaidi barani kote. Aflasafe ni kidhibiti asilia cha kibaiolojia kinachotayarishwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) na washirika wake ili kukomesha uchafuzi unaotokana na aflatoksini, Pia, tunakuza maendeleo yake, maendeleo haya yanaweza kuhamishwa kwenye sekta ya kibinafsi na kutumika katika maeneo mengi, hii ina maana kwamba kazi zaidi zitapatikana katika sekta za ujenzi, utengenezaji bidhaa na uchunguzi maabarani.

Bidhaa hizi mbili zinaweza kuongeza ugavi wa chakula- kupitia ongezeko la mazao au upunguzaji wa hasara- na hivyo basi kuchochea fursa zaidi za kibiashara.

Miradi zaidi ambayo ingali inashughulikiwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) ni mfumo vumbuzi wa uzalishaji samaki na shughuli za uchakataji chakula kutoka mimea ambayo utafiti wetu unalenga, mimea hii ni: muhogo, maharagwe ya soya, nafaka ya cowpea, viazi na ndizi.

Kutumikiza Jukwaa letu la Ukuzaji katika Biashara pia kuna maana ya kwamba watu binafsi wanafanya kazi kwenye mtandao mkubwa, hii ni pamoja na kukutana na washirika, wafadhili wanaoweza kufadhili baadhi ya miradi na watu wengine wanaoweza kuleta manufaa kwa baadhi ya miradi. Hii inajumuisha kushiriki kwa uvumbuzi au huduma za kutoa mkopo kuweza kufikia utambuzi na uimarishaji wa masoko mapya ya vifaa na mimea maalum. Hivi “viunganishi” vinatokana na motisha kwamba kilimo sio hatima ya kizazi kilichopita cha watu maskini lakini eneo la kufurahiwa ambalo linaweza kuliwezesha bara la Afrika kulitumikiza kundi lake kubwa la watu: ambalo linajumuisha vijana.

Waundaji sera wana mengi ya kufanya ili kukuza mazingira yafaayo kwa wakulima wadogo kunawiri, mazingira hayo lazima yajumuishe watu, na hili ndilo tunalojaribu kufanya.

(Mwisho)